

Octoba 23, 2019

Kijarida cha Mountain View

Ujumbe wa Mwalimu Mkoo

Nataka kuwashukuru wale waliojali kwenye mkutano wetu wa Baraza la Jamii ya Shule mnamo ijumaa iliyopita. Sauti za wazazi ambao waliojali inachangia ili kudumisha ubora wa shule yetu na kuchangia katika kufanya iwe bora hata zaidi. Tunathamini maoni na kujitolea kwako. Wanachama wetu ambao ni wazazi ni Viridiana Cardenas, Nichole Swink, Yesica Torres, Amy Jordan, Osman Osman, na Miriam Landeros. Uhaweza kushauriana na yeoyote ya wazazi hawa ikiwa una wasiliasi au maswali yanayohusiana na Mountain View, na watakuwakilisha kwenye Baraza la Jamii ya Shule.

Maonyesho ya Kutisha ya Halloween

Tunafurahi kutangaza Fair ya Halloween ya Scare ambayo itafanyika Ijumaa, Oktoba 25 kutoka 3:00 hadi 6:00 pm katika Kituo cha Kujifunza Jamii. Kutakuwa na uchunguzi wa kiafya, rasilimali za afya za jamii, shughuli za watoto, kibanda cha kupigwa picha, na vitisho vya kupata peremende. Mojawapo ya hali za kufurahisha za tukio hili ni kwamba wewe na familia yako mnaweza kuja kupata chanjo za homa bila malipo! Chanjo hizi zitapatikana bidhaa zikipatikana kati ya 12:00 na 6:00 pm Lazima wapokeaji wa change wawe na umri wa angalau miaka misaba. Tunahimiza kila mtu kushiriki. Kuwa mgonjwa hugharimu familia pesa, muda, na wasilasi. Epuka magonjwa nyumbani mwako kwa kupata change. Tunataka kushukuru Walgreens, Wakfu wa Elimu wa Salt Lake, na Shirika la Afya ya Jamii la Utah kwa kufanya tukio na chanjo hizi ziwezekane.

Sherehe za Halloween mnamo Octoba 31

Nimeweka maswali machache kuhusu Halloween. Mnamo Oktoba 31 tutakuwa na siku kamili ya shule. Wanafunzi wanaweza kuleta mavazi yao shulen, na tutaandaa gwaride la wanafunzi ili kuonyesha mavazi yao na kuona mavazi ya wengine. Gwaride hilo litafanyika saa 1:30. Tafadhalii ruhusu gwaride lipite vizuri bila kuwachukua wanafunzi ili kwenda kupigwa picha. Wanafunzi wataweza kupiga picha mwishoni mwa gwaride na baada ya shule. Tafadhalii fahamu kuwa tunao baadhi ya wanafunzi wachanga ambao wanaweza kutisha kwa urahisi. Tafadhalii hakikisha kuwa mavazi ya mtoto wako sio ya kutisha au ya umwagaji damu, na kwamba hawataleta silaha yoyote halisi au bandia, hata ikiwa zinaingiana na mavazi. Vinyago na kofia zitaruhusiwa tu wakati wa gwaride na lazima ziondolewe kabla na baada ya gwaride. Wazazi wandakaribishwa kwenye gwaride hili, na wanatarajwa kufuata maagizo ya shule ya kuwa salama, kuonyesha heshima, uwajibikaji, na kujali wanapokuwa shulen.

Hakuna mwajiriwa au mwanafuni wa wilaya atakayebaguliwa katika ajira au programu au shughuli yoyote ya wilaya kwa misingi ya umri, rangi, ulemau, jinsia, taarifa za vinasaba, uifa, ujauzito, mbari, dini, utambulisho wa kingono, au hali ya ustaaufu. Wilaya imedhamiria kutoa ufikio sawa na fursa sawa katika programu zake, huduma na ajira ikiwemo sera zake, michakato ya malalamiko, ufikiaji wa programu, matumizi ya huduma za wilaya, malazi na masuala mengine ya Fursa Sawa za Ajira. Wilaya pia inatoa ufikio sawa kwa huduma za wilaya kwa makundi yote ya vijana yaliyoordheshewa katika Title 36 ya Sheria ya Marekani, ikiwemo makundi ya skauti. Mtaa afuataye amechaguliwa kushughulikia maulizo na malalamiko kuhusiana na masuala ya ubaguzi, unyanasaj, na ulipizi ulio kinyume na sheria: Tina Hatch, Utii na Uchunguzi, 440 East 100 South, Salt Lake City, Utah 84111, (801) 578-8388. Unaweza pia kuwasiliana na Ofisi ya Haki za Kirala, Denver, CO, (303) 844-5695.



Matukio Yanayokuja

Ijumaa, Oktoba 25

Chanjo Isiyolipishwa ya Homa, 12:00-6:00, CLC

Ijumaa, Oktoba 25

Maonyesho ya Kutisha ya Halloween, 3:00-6:00, CLC

Jumatano, Oktoba 30

Ziara ya Kimasomo ya Darasa la Chekechea Ziara Kwenda Shambani

Alhamisi, Oktoba 31

Ziara ya Kimasomo ya Daraja la Tano, Chuo Kikuu cha Utah (Asubuhi)

Alhamisi, Oktoba 31

Gwaride la Halloween, 1:30

Mkutano wa Ushauri kwa Wazazi

Kila asubuhi ya Ijumaa wazazi wana nafasi ya kujifunza kuhusu mfumo wa elimu, kukutana na kitivo na wafanyakazi wa shule, na kujadili masuala muhimu katika uzoefu wa watoto wao shulen. Tunakualisha ufike siku ya Ijumaa na uwe sehemu ya majadiliano haya. Tunakutana saa 8:15 katika Kituo cha Masomo cha Jumuiya, Chumba 182. Ikiwa unahitaji msaada kukiipa, wafanyakazi wetu katika ofisi watakusaidia kupata maeleko ya njia sahihi. Natumai kukutana nawel!

Baraza la Jumuiya ya Shule

Baraza la Jumuiya ya Shule (SCC) itakutana kila mwezi katika CLC. Mikutano ya SCC ni wazi kwa umma.

Fuata au Uwe Rafiki wa Shule ya Mountain View kwenye Mitando ya Kijamii

Facebook: @MountainViewSLC

Twitter: @mtviewlibrary

Tunatarajia kuwa utatufuata, na tunatumai kuwa utadilika jamaa na marafiki ili kutufuata, pia.

Masomo ya Kituo cha Mafunzo cha Jumuiya

Kituo chetu cha Mafunzo cha Jumuiya kinatoa masomo mengi kwa ajili ya wahafunzi na watu wazima. Tafadhalii tembelea ofisi za Kituo cha Kujifunzia Jumuiya ili ujipatie kalenda husika.

Mtu yeoyote wa jumuiya yetu anakaribishwa kujianidikisha na masomo.

MV LIMB Newsletter 102319 SWAHILI 2019-10-21